# LEARNING BY EAR

# ”If a tree falls… - Deforestation in Africa"

**EPISODE SEVEN: "Local Solutions"**

**AUTHOR: Romie Singh**

**EDITORS: Thomas Mösch, Jan-Philipp Scholz**

**PROOFREADING: Natalie Glanville-Wallis**

**List of characters EPISODE SEVEN:**

**Narrator**

| | |
|---|---|
| **SCENE 1** | **Talib (m, 20) Mother (f, 36) Isi (m, 18) Group of Men/Women** |
| **SCENE 2** | **Chika (f, 18) Mother (f, 36) Isi (m, 18) Group of Women** |
| **SCENE 3** | **Mulogo (m, 22) Chika (f, 18) Talib (m, 20)** |
| **SCENE 4** | **Mulogo (m, 22) Talib (m, 20)** |
| **SCENE 5** | **Mother (f, 36) Chika (f, 18) Group of Women "Themba" (f, 30)** |
| **SCENE 6** | **Mulogo (m, 22) Chika (f, 18) Talib (m, 20)** |
| **SCENE 7** | **Isi (m, 18) Mother (m, 36) Chika (f, 18) Akiki (f, 7)** |
| **SCENE 8** | **Mulogo (m, 22) Chika (f, 18)** |

## INTRO

Karibu kwenye *Noa Bongo Jenga Maisha Yako* na katika kipindi cha saba cha mchezo wetu mpya kuhusu uharibifu wa misitu.

Kisa hiki kinaendelea kwenye mazingira ya vita vya wenyewe kwa wenyewe na kinaonyesha jinsi uharibifu wa misitu- ukataji wa miti na maeneo ya nyasi- ulivyotatiza maisha ya vijijini na kusababisha mzozo kati ya jamii mbili za wakulima. Sasa jamii hizo mbili zinajipata pamoja kwenye kambi ya wakimbizi ya Dovani na zimeanza kutafuta ufumbuzi sawa kwa matatizo ya siku za usoni.

Katika kipindi cha leo, kina mama wanatoa taarifa ya upandaji wa mimea na pia kuhusu mimea ya dawa ambayo ingali mwituni. Wakati huo huo hali ya taharuki imetanda katika kambi ya Dovani. Akiki ametoweka. Je atampata dada yake?
Jiunge nasi umsikie Talib akieleza jinsi Akiki alivyotoweka ghafla.

**Episode SEVEN: "LOCAL SOLUTIONS."**

**<u>1.MUSIC UP</u>**

**<u>Scene 1</u>**

**2.TALIB NARRATOR:** Habari zenyewe zilitushtua si haba. Akiki alikuwa ametoweka. Kitu cha kwanza tulichokisikia jana usiku ni Mama Kipko na Isingoma wakipiga mayowe....

**<u>3.INSERT: FADE IN SFX EVENING AMBIENCE/HOLD MUSIC UNDER</u>**

**4.MOTHER: (very upset)** Akiki? **(sobbing)** Isi? Yuko wapi? Na giza lote hili. Ng’ombe wake yuko hapa lakini mwenyewe hayupo.

**5.ISI:** Sijui ma. Nitakwenda kumtafuta. Usiwe na wasiwasi!

**6.ISI RUNNING CALLING OFF MIC:** AKIKI! AKIKIKI!

**7.MOTHER CALLING OFF MIC:** AKIKI! AKIKI

**<u>8. Background voices of men and women asking what’s wrong</u>**

**9.MOTHER: screaming** Akiki ametoweka! Ametoweka!

**<u>10.FADE SOUNDS. END OF INSERT</u>**

**11.TALIB NARRATOR:** …Tuliwafahamisha wakazi wengi wa kambi ya Dovani na kila mtu akajiunga na shughuli ya kumtafuta. Lakini hatukumpata. Mama Kipko na Isingoma ndio walioumia zaidi kwa kuwa walikuwa wamemchukua Akiki ili wamlee. Sasa kina mama wote akiwemo Chika wanahamasishana kuwasaidia watu hao wawili.

**Scene 2**

**12.SFX Morning ambience outside**

**13.WOMEN'S VOICES CONSOLING MAKIPKO:** Usijali ma; yuko sawa; ni mtoto mwerevu.

**14.MOTHER:** Lakini kwa nini atoroke? Amekwenda wapi?

**15.ISI:** Ma, nadhani alipata fikra ya hadithi uliyomsimulia kuhusu mzee aliyejifisha kwenye mbuyu. Akiki anafikiria huenda dadake amejificha kwenye mbuyu katika Abanto.

**16.MOTHER:** Mungu wangu. Amekwenda huko kweli?

**17.CHIKA: (gently)** Hakuna ajuaye Ma Kipko wala kusimama tu hapa hakusaidii vyovyote. Wanaume wanamtafuta kwa magari. Tafadhali nenda nyumbani.

**18.CHORUS OF WOMEN ALL AGREEING NOT TO WORRY**

**19.CHIKA:** Eee. Kina mama wenzangu. Tulisema tutakusanya mimea na mizizi ya dawa tuipeleke kwenye zahanati yetu. Tunapaswa kutoa taarifa ya vitu tulivyopata. Je mko tayari kuandamana nami? Ninapaswa kuandika kumbukumbu za kikao kilichopita.

**20.WOMEN** Naam Chika. Twende. Hakuna tatizo. Twendeni.

**21.MUSIC UP**

**Scene 3**

**22.SFX Morning ambience outside**

**23.MULOGO:** Hujambo Chika. Mbona hivyo? Hujachangamka. Nikuchangamshe?

**24.CHIKA:** Sijambo Mulogo! Ninapaswa kuandika kumbukumbu za mkutano uliopita. Lakini unaweza kunitayarishia chai ikiwa unataka.

**25.MULOGO:** Kwa kutumia "jiko la kombora"?

**26.CHIKA: (laughing)** Naam…tunalizungusha jiko hilo kwa kila mtu ili sote tuweze kulitumia. Leo ni zamu yangu. Unaweza kulishughulikia?

**27.MULOGO:** Bila shaka. Endelea na kazi yako. Mimi nitashughulika huku kwengine!

**28.SFX: Grass, wood, striking of match**

**29.MULOGO:** Nimelipenda! Ni safi kuliko jiko zee la makaa tulilokuwa nalo nyumbani. Kumbe babangu ana akili pevu!

**30.SFX flames burning sticks**

**31.MULOGO:** Sikiza Chika! Najua pengine huu si wakati mwafaka...

**32.CHIKA:** ehe

**33.MULOGO: (laughing)** Ninafikiria kuhusu siku za usoni....

**34.TALIB (OFF MIC)** Aaha. Nimeshakupata Chika! Oh… Mulogo hujambo! Unapika chai? Vyema! Au ninawatatiza?

**35.CHIKA: (embarrassed)** aah..ummm…la..hapana Talib. Hata kidogo! Mkutano wa kina mama ni hivi karibuni. Ebu nikafanyie kazi zangu ndani. Nyie wawili mnaweza kuzungumzia hapa nje!

**36.SFX: FOOTSTEPS DEPARTING**

**Scene 4**

**37. SFX Same ambience as Scene before (morning ambience)**

**38.TALIB:** Samahani. Nimekuja wakati usiofaa. Sikujua kwamba wewe na yeye.... mmm...sawa....hayanihusu. Ama niseme yananihusu. Mimi na Chika tunafanya kazi na tunashirikiana vyema. Singependa hali hiyo ibadilike.

**39.MULOGO:** Ati? Na kwa nini hali ibadilike?

**40.TALIB:** Sikiza…mimi…ninampenda Chika sana.

**41.MULOGO:** Woa..acha hayo. Habari nyingi sana hizo. Nimekuja kuzungumza na Chika.... kusema nina mipango ya siku za usoni …

**42.TALIB:** Naam, kwa hivyo nimekisia sawa... nina sababu ya kuingiwa na wasiwasi.

**43.MULOGO:** Ati nini? Hapana! Sizungumzii HILO! Nazungumzia kupanga mkutano.

**44.TALIB:** Mkutano?

**45.MULOGO:** Naam, nikutane nanyi!

**46.TALIB:** Nasi?

**47.MULOGO:** Naam! Pamoja na *Saidia Afrika*. Nadhani Chika alinielewa visivyo.

**48.TALIB:** oooh. Na kwa nini akuelewe visivyo?

**49.MULOGO:** Hilo, muulize wewe mwenyewe. Sikiza….acha niongeze vijiti zaidi kwenye moto.

**50. SFX: Sticks/flames**

**51.MULOGO:** Naam! Sasa hivi! Ndo hayo ninayotaka kusema. Ningependa kujua jinsi mnavyofanya kazi. Nina mawazo mazito! Wazo MOJA zito! Nataka kujua ikiwa *Saidia Afrika* INASAIDIA kweli au la!!

**52.TALIB:** Basi tutazungumza baadaye wakati Chika akiwa na nafasi zaidi, baada ya mkutano wa kina mama.

**53.MUSIC UP**

**Scene 5**

**54. SFX Daytime ambience**

**55.MOTHER:** Kina mama wenzangu. Karibuni. Ninawashukuru sana kwa msaada wetu wa leo asubuhi. Siwezi kubakia nyumbani nikilia.

**56.WOMEN MURMUR IN APPROVAL**

**57.MOTHER:** Nani atajitolea kuandika kumbukumbu?

**58.WOMEN MURMUR:**

**59.CHIKA:** Themba? Naona umeinua mkono.

**60.THEMBA:** Naam! Nitaandika.

**61.CHIKA:** Asante sana! Jambo zuri hilo! Nyote mtahitajika kuwa na uzoefu wa haya mambo baadaye wakati mtakapokuwa mkishauriana na wadau wa misitu pamoja na serikali kuhusu haki za ardhi. Kwa hivyo anzeni kufanya mazoezi! Mara ijayo utaandika wewe, Alice, sawa?

**62. SOFT LAUGHTER AMONG WOMEN**

**63.MOTHER:** Haya! Kulingana na orodha ya mada za leo, tuna taarifa mbili: moja kutoka kundi la kupanda maharagwe ya soya na ya pili ya kundi la mimea ya dawa. Natumai, Chika, utaanza wewe.

**64.CHIKA:** Ndio! Sawa! Leo asubuhi tulimaliza kupanda safu kumi za maharagwe ya soya. Ni msimu wake huu. Ni bora kwa kuwa tuliongeza samadi. Udongo ulikuwa mgumu sana kabla ya upanzi.

**65.THEMBA:** Safu zenyewe zinapendeza si haba!

**66.MOTHER:** Mimea itakapokua itashikana na kufunika maeneo ya safu yaliyo wazi. Hali hiyo itayasaidia mazao kukua vizuri.

**67.CHIKA:** Na ule mtambo ambao Shirika la *Saidia Afrika* lilituahidi ili kukonyoa maharagwe hayo kwa ajili ya mafuta, utatusaidia sisi kujitengenezea mafuta ya kupikia.

**68.MOTHER:** Habari zote nzuri hizi! Asante. Na kutoka kwa kina mama waliokwenda msituni?

**69.CHIKA:** Kina mama hao walileta vikapu sita vya magome ya misufi, minanaa na tangawizi. Jambo la kutia moyo ni kwamba maeneo ya misitu upande wa magharibi hayajaharibiwa sana. Tusipoharibu misitu, tutaendelea kupata miti mingi ya dawa kutegemea mahitaji yetu.

**70.MOTHER:** Asante kina mama wenzangu, kwa shughuli nzuri hiyo ya siku ya leo.

**<u>71. FADE ON WOMEN CLAPPING</u>**

**Scene 6**

**72. SFX Daytime ambience outside**

**73.MULOGO:** Hatimaye, Huyo Chika anakuja. Mkutano umekuwa vipi?

**74.CHIKA:** Umekuwa mzuri! Tumepiga hatua kubwa.

Kwani ninawatatatiza?

**75.MULOGO:** Hapana, la hasha. Tafadhali Chika. Keti. Ningependa kujua kutoka kwako na Talib ikiwa shirika la *Saidia Afrika* pia husaidia kuanzisha miradi inayolengwa kuleta faida na kipato katika jamii.

**76.CHIKA:** Sidhani kama tuna fedha. Tunahitaji ufadhili na inatubidi kuwategemea vigogo wafadhili miradi yetu.

**77.TALIB:** Lakini huwa twazungumza kuhusiana na jinsi ya kuwa na ubia. Kwani una fikra gani?

**78.MULOGO:** Tunajua matumizi ya kienyeji ya kuni kupikia yanaangamiza misitu yetu, na pia kutumia kuni nyumbani kunasababisha matatizo ya kupumua hasa kwa kina mama wanaopika .

**79.CHIKA:** Na kwa watoto wao pia.

**80.TALIB:** Sawa, lakini pia kuna sababu za kimazingira. Usisahau jinsi miti yetu ilivyo muhimu kwa maji yetu, kwa makazi au mimea na ng'ombe. Husaidia kutupatia hewa safi..

**81.MULOGO:** Wewe na Chika mlinifahamisha hayo kitambo. Lakini ili tuokoe miti, tunahitaji nishati mbadala ambayo ni safi. Nimesoma kwamba tunaweza kuchoma takataka- kinyesi cha ng’ombe, choo cha binadamu, mimea iliyochakaa- kwa kiasi cha kusaidia jamii ndogo. Acha niwaonyeshe. Tizameni hapa.

**82.SFX PAPER NOISE**

**83.CHIKA:** Naam. Mimi na Talib tumekuwa tukizungumza kuhusu mitambo hii ya kutengeneza nishati mbadala. Tuliwahi kutembelea mradi kama huu. Mtambo huo ulikuwa umejengwa chini ya ardhi na gesi ilitokana na huo mchakato wa kuchoma taka. Gesi hiyo ilitumiwa kuwashia taa na pia kupikia chakula.

**84.MULOGO:** Uzuri wake, ni kwamba, ni safi na rahisi kupatikana kwa jamii za vijijini. Haina madhara kwa mazingira. Sikizeni! Kwa mujibu wa takwimu, mtu anahitaji kati ya shilingi elfu arobaini na elfu themanini kuunda mtambo mmoja kama huo barani Afrika.

**85.TALIB:** Hmm. Unataka kujua ikiwa shirika la *Saidia Afrika* linaweza kuwekeza kwenye mradi kama huo..

**86.CHIKA:** … na kufadhili mradi wa kijamii unaoleta faida.

**87.MULOGO:** Tuseme hivyo, Naam.

**88.CHIKA:** Kama yalivyo mambo mengi Mulogo, mtu anahitajika kuandaa mpango mzuri ambao hauna gharama kubwa.

**<u>89.MUSIC UP</u>**

**<u>Scene 7</u>**

**<u>90. SFX Evening ambiecne / Sound of lorry approaching</u>**

**91.ISI:** Kuna nini? Lori? Wakati huu?

**<u>92.ISI PANTING AND RUNNING / LORRY ENGINE BECOMES LOUDER</u>**

**93.MOTHER: (OFF MIC)** Mimi pia nimelisikia. Dereva yule pale. Muulize.

**94.ISI: (shouting above the engine)** Vipi…Umemuona msichana mdogo?

**95.MOTHER:** Hawezi kukusikia. Tazama...kule! Ndiye yule- Ni Akiki....ameandamana na mtu mwingine... ni msichana.

**<u>96.SFX RUNING AND PANTING</u>**

**97.CHIKA:** Mama Kipko**…**Isi…yuko salama. Akiki yuko salama….

**98.ISI:** Tumshukuru Mungu.

**99.MOTHER: (sobbing)** Akiki kipenzi changu!

**100.AKIKI: (joyful)** Ma! Nimempata…kama kwenye ndoto yangu…dereva alinipeleka huko!

**101.ISI:** Sesi? Umempata dadako Sesi aliyetoweka?

**102.MOTHER:** Na mume wangu? Wanangu?

**103.ISI:** Kato? Ulimuona ndugu yangu Kato?

**104.CHIKA:** Shh. Itawabidi mngoje. Sesi bado amechanganyikiwa. Hawezi kuzungumza. Dereva ameniambia walimpata akiwa amejikunyata kwenye mti. Akiki alijua mahali pa kwenda kumtafuta.

**105.AKIKI: (sounding very weak and tired)** Naam. Nilijua alikokuwa. Isi, Nimempata. Kama Ma alivyosema. Katika mti wa mbuyu!

**SCENE 8**

**106. SFX Same ambience as before**

**107.MULOGO: (gently)** Njoo Chika.

**108.CHIKA: (Gentle/surprised)** Mulogo!

**109.MULOGO:** Nitapika chai tunywe tupate joto kidogo.

**110.CHIKA:** Ndiyo..asante. Napenda hivyo. Usiku wenyewe umekuwa mrefu. Nafurahi umekwisha vizuri!

**111.MULOGO:** Naam..lakini ningependa kuongea nawe... kuhusu sisi wawili.

**112.MUSIC UP**

**OUTRO.**

Ni hayo tuliyokuandalia kwa leo katika kipindi cha *Noa Bongo Jenga Maisha Yako* kiitwacho "Mti unapoanguka...", kilichoandikwa na Romie Singh, unaoshughulikia suala la uharibifu wa misitu. Sesi amerejea salama lakini ametatizika kiasi cha kushindwa kuongea. Katika kipindi chetu kijacho,Isi anaona kwamba kuwa yeye ni pacha kumesababishia familia yake laana. Lakini kina mama wanajitahidi kuunda shirika jipya la umoja wa jamii.
Usikose kujiunga nasi katika kipindi cha nane upate kujua mambo yatakavyokuwa.
Kumbuka, ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki au kuwaarifu marafiki zako kukihusu, tafadhali tazama wavuti wetu www.dw-world.de/lbe

Kwaheri kwa sasa!

**END OF EPISODE 7**